

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

Telegramu: "LEGAL"
Simu Na.: +255 26 2310019
Nukushi: +255 26 2310056
Barua Pepe: km@sheria.go.tz
DodomaTovuti: www.sheria.go.tz



Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Katiba,
S. L. P. 315,
40484 DODOMA

TAARIFA KWA UMMA

**MAWAZIRI WA SHERIA WA UMOJA WA AFRIKA WARIDHIA ITIFAKI MBILI ZA
KIUCHUMI**

Durban, Afrika Kusini - 10 Februari, 2024

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (MB) amesema itifaki mbili za Biashara Mtandao na Wanawake na Vijana katika Biashara zimeridhiwa na Mawaziri wa Sheria wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika na sasa itifaki hizo zinatarajiwa kuwasilishwa katika mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali baadae mwezi huu kwa ajili ya kupitiwa na kuridhiwa ili zianze kutumika rasmi.

Waziri Pindi Chana ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri wa Sheria ya Umoja wa Afrika ameyasema hayo leo tarehe 10 Februari, 2024 wakati akifungua Mkutano maalum wa Tisa wa Kamati ya Watalaam na Mawaziri wa sheria na Haki ya Umoja wa Afrika, 2024 Jijini Durban, Afrika Kusini.

Waziri Chana amesema tarehe 22 Januari, 2024 alipokea nakala ya barua kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Mawaziri ya Viwanda na Biashara ikimfahamisha kuwa Mkutano wa 12 wa Kamati Maalum ya Mawaziri wa Biashara na Uchumi ya Umoja wa Afrika imeridhia itifaki mbili ambazo ni Itifaki ya Biashara ya Mtandao na Itifaki ya Wanawake na Vijana katika Biashara na wakaomba Kamati ya Mawaziri wa Sheria kuzipitia na kuziwasilisha katika mkutano mkuu.

Kutokana na umuhimu wa itifaki hizi hasa katika kukuza uchumi wa Bara la Afrika, Waziri Chana aliandika barua kwenda kwa Ofisi ya Sheria ya Umoja wa Afrika ili kuwasilisha ombi la Tanzania kuitisha mkutano maalum wa Tisa unaoendelea hivi sasa ambapo zaidi ya nchi 40 ziliridhia na hivyo kuwezesha mkutano huo kufanyika.

Aidha, Mwenyekiti Pindi Chana ameishukuru Serikali ya Afrika Kusini na kipekee Rais Cyril Ramaphosa kwa kuridhia Mkutano huu kufanyika katika jiji la Durban Afrika Kusini na akatumia nafasi hiyo kuwaalika wajumbe hao katika Mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola unaotarajiwa kufanyika Unguja Zanzibar tarehe 04 – 08 Machi, 2024.

Lusajo Mwakabuku

MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI